# Changamoto za Kuueleza Msamiati wa Samaki: Mtazamo wa Kiuhusiano

*John Habwe, Rayya Timammy na Amir Swaleh*
*Chuo Kikuu cha Nairobi*

**Ikisiri**

**Makala haya yanachunguza maelezo ya majina ya samaki katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Kwa kutumia nadharia ya kiuhusiano imebainika kuwa kunatumika vichocheo au mikakati tofauti tofauti ili kumweleza samaki. Hata hivyo, licha ya vijenzi hivi kutumika bado kuna changamoto nyingi kama vile maelezo fulani kukosa uangavu kwa kuwa ni mapana zaidi au kutochangia kikamilifu katika kumweleza samaki kwa kuwa ni maelezo finyu, kutotumia vichocheo vya kutosha au kichocheo kimoja ambapo vichocheo vingi vingefaa zaidi. Aidha, imebainika kuwa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (KKS) imetumia vichocheo vya tabia, chakula, rangi, umbo, vumba na hata picha ili kuwaeleza aina ya samaki ili wasomaji waweze kuwatambua na kuwaeleza. Licha ya vichocheo hivi, ni wazi kuwa KKS bado inakabiliwa na changamoto ya kuwaeleza samaki kwa uwazi, uangavu na kwa kukinaisha.**

**Maneno Muhimu:** *Msamiati wa Samaki, Changamoto, Kiuhusiano*

## Utangulizi

Makala haya yanaangazia baadhi ya changamoto zinazofungamana na ufafanuzi na ufasiri wa viumbe wa majini. Ingawa viumbe wa majini ni wengi mno na wa aina mbalimbali kama vile kiboko, mamba, kambakoche, nyoka, kaa, n.k., tutajikita katika maelezo ya samaki pekee. Tumechanganua majina thelathini ya samaki.

Kumekuwa na maendeleo makubwa katika uwanja wa leksikografia katika Afrika Mashariki ambapo kumejitokeza makamusi ya aina mbalimbali. Kuna makamusi ya lugha moja, lugha mbili, makamusi ya watoto, ya kitaaluma, ya visawe, ya semi, ensaiklopidia na makamusi sanifu. Hata hivyo, tutajikita katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu (KKS) iliyochapishwa na Oxford University Press (OUP, 2014), toleo la tatu. Tunachukulia kwamba kamusi hii ndiyo maarufu zaidi kwani ina usomaji mpana sana hasa miongoni mwa wanafunzi katika eneo la Afrika Mashariki.

Lengo kubwa la kamusi kama kitabu cha rejea huwa ni kueleza maana ya vidahizo fulani ili vieleweke barabara kwa kutumia sifa bainifu (Zgusta, 1971). Kwa mujibu wa nadharia ya kiuhusiano ya Sperber na Wilson (1995) na Wilson na Sperber (2004), hii ni shughuli ya kimawasiliano na kiutambuzi kuhusu namna

mwandishi anavyowasilisha maelezo ya vidahizo na vichocheo vya kuyafasiri maelezo hayo ili yapate kueleweka. Vichocheo au maelezo hayo hupimwa kwa misingi ya muktadha wa kisaikolojia ambao unajumuisha mambo yote ambayo msikilizaji au msomaji anayajua kama vipengele vya utamaduni, habari za awali kuhusu shughuli fulani na mambo yaliyo katika mazingira ambayo ndani yake wanatagusana. Kamusi ya KKS inalenga wasomaji wa takriban viwango vyote. Kwa sababu hii maelezo ya viumbe wa baharini yanafaa kuafiki mahitaji ya watoto, watu wazima, wazalia au wenyeji wa lugha ya Kiswahili na watumiaji wengine wa lugha hii ikiwa kama lugha ya pili, ya tatu au hata ya nne. Katika kutoa maelezo haya kamusi hutumia mikakati kadha wa kadha ili kufanikisha lengo hili la kueleweka. Baadhi ya mikakati inayotumiwa katika kamusi hii sanifu tutaijadili baadaye katika makala haya. Mikakati hii tunairejelea katika makala haya kama vichocheo ambavyo vinamsaidia mfasiri wa maana inayoelezwa na mwandishi na ambayo imelengwa yeye aielewe. Sehemu ifuatayo inajadili nadharia iliyotumika katika kazi hii.

**Nadharia ya Uhusiano ya Dan Sperber na Deirdre Wilson**

Kwa kuwa tunashughulikia maswala ya uelezaji au ufasiri wa vidahizo katika kamusi, tumetumia Nadharia ya Kiuhusiano iliyoasisiwa na Dan Sperber na Deirdre Wilson (1995) na Wilson na Sperber (2004). Nadharia hii inadai kuwa mawasiliano yoyote baina ya binadamu yamelengwa katika kuyafanya mambo yote yanayosemwa kuwa ya kiuhusiano zaidi. Hali hii inakuwa hivi ili mambo yanayosemwa yapate kueleweka na msikilizaji au msomaji aliyelengwa. Hii ni kwa sababu kuwa ubongo wa binadamu una shughuli nyingi na wakati wa mawasiliano hulenga kuteua usemi ambao ni wa kiuhusiano zaidi na ambao utasaidia katika kulielewa lengo au azma ya msemaji au mwandishi wa ujumbe bila matatizo.

Nadharia hii ni tofauti na Nadharia ya Umaanisho ya Grice (1975) ambapo kanuni ya mawasiliano, kwa mfano, huvunjwa na msemaji aliye na jukumu la kumweleza msomaji au msikilizaji wake ujumbe fulani. Nadharia hii ya Kiuhusiano ni ya kiutambuzi (Wilson na Sperber (1995), Carston (1988), Sperber (1996) na Unger (2001). Hii ina maana kuwa vichocheo anavyotoa msemaji au mwandishi huvitoa kimaksudi kwa lengo la kuathiri ufasiri wa ujumbe wake kwa upande wa msikilizaji au msomaji.

Grice (1975) anadai kuwa lugha huwa na semi za aina mbili zi1izosemwa moja kwa moja na nyingine zilizo fiche zaidi. Zilizosemwa moja kwa moja, kwa mujibu wa Grice, hazihitaji ufasiri kwa kuwa zimefuata kanuni za lugha ipasavyo au kwa usemi wa Grice, zinafuata kanuni nne za ushirikiano ambazo ni kanuni ya idadi, ukweli, uhusiano na ile ya namna. Lakini kwa upande mwingine, kuna zile semi ambazo hazifuati kanuni hizi kama vile matumizi ya methali, sitiari tamathali zingine zozote na matumizi yote ya mafumbo ambayo huhitaji ufasiri.

Grice (1975, 1989) anasisitiza kuwa ili kuelewa semi hizi fiche muktadha huwa ni muhimu. Hata hivyo, Sperber na Wilson (1995) kwa kutumia mtazamo wa

kiutambuzi, wanadai kuwa aina zote mbili za semi fiche na wazi, zinahitaji ufasiri wa aina fulani ili kuweza kueleweka ipasavyo. Kulingana na nadharia ya kiuhusiano, matumizi ya lugha iliyo wazi huhitaji viungo fulani ili kuzitajirisha semi husika. Jambo hili huweza kufanyika kwa kuzipanua, kuzibana au kuzifanyia ukadiriaji. Kwa mfano, viwakilishi kama vile yeye, hiki n.k. na sifa za kiusonde zikitumika lazima zitajirishwe na msikilizaji au msomaji ili wazo lililolengwa lieleweke barabara. Ufundi huu wa utajirishaji utakuwa muhimu sana kwetu kwani maelezo ya kamusi hii hutumia mkakati ulio wazi au eksiplikecha.

Kwa mujibu wa nadharia ya kiuhusiano, mwandishi huhakikisha kuwa ameieleza habari yake kwa namna ambayo itakuwa rahisi kueleweka na msomaji wake; yaani itakuwa haina gharama kubwa wakati msomaji atakapokuwa anaifasiri. Kwa mujibu wa Unger (2001) kila msemaji huhakikisha kuwa anachotaka kusema au kukiandika kina sifa kubwa za kiuhusiano kwa kuwa na vichocheo vya kutosha vya kumwezesha kuwasiliana kwa njia bora zaidi. Lakini mwandishi asipozingatia mikakati hii ya kimawasiliano, huenda mfasiri wake akashindwa kukielewa alichokilenga kumweleza. Kwa upande mwingine msomaji au msemaji hutumia kanuni ya uhusiano kuchuja maelezo yanayotolewa ili kuona yanavyoingiliana na kile anachokijua au hata kukiamini (Marmardou, 2000).

Waandishi wa makamusi aghalabu huhakikisha wamefafanua kidahizo cha kamusi kwa namna ambayo itakuwa na uhusiano mkubwa kwa msomaji wao. Kwa maneno mengine, maelezo ya kamusi lazima yachukulie kuwa yana kiwango kikubwa cha uhusiano kinachoweza kumfanya msikilizaji kutotatizika wakati wa ufasiri wake wa kile kilicholengwa na mwandishi. Kwa mujibu wa nadharia ya kiuhusiano msemaji huwa analenga kuzua vichocheo ambavyo vina uhusiano mkubwa ili usemi au maelezo fulani yapate kufasiriwa kwa njia bora kabisa.

## Mbinu za Utafiti

Data ya utafiti huu ilikusanywa makatabani ambapo tulijikita katika maandishi yaliyomo katika kamusi ya KKS. Tulichagua kamusi ya KKS kwa sababu ina usomaji mpana zaidi na hutumiwa na wanafunzi, walimu na watumiaji wengine wa lugha kwa kiwango kikubwa. Toleo la kwanza la Kamusi hii lilichapishwa mwaka wa 1981 lakini tumeshughulikia kongoo la toleo la tatu (2014). Hili ndilo lililorekebishwa na kuboreshwa zaidi kwa kuyafanya maelezo yawe wazi kwa wasomaji.

Tumesoma vidahizo vilivyolenga kuwaeleza samaki kisha tukateua kimaksudi vidahizo ambavyo vingetufaa zaidi katika utafiti huu. Baadaye tukavichanganua kwa kutumia nadharia ya kiuhusiano ambayo imelenga kuonyesha ufaafu wa vichocheo hivyo.

**Vichocheo vya Kamusi**

Katika sehemu hii tunajadili baadhi ya vichocheo au mikakati iliyotumiwa kuwaeleza samaki katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu (KKS). Tutaanza kujadili kichocheo cha maumbile au umbo la samaki kwa kuwa ndicho kinachotumika zaidi katika maelezo mengi ya samaki. Mbali na kichocheo hiki cha kimaumbile kunatumika vichocheo vingine vya vumba, rangi, tabia, makazi na picha. Lazima ikumbukwe kwamba, KKS mara nyingi imetumia vichocheo vingi kwa pamoja ili kuboresha maelezo na kurahisisha utambuzi wa msomaji.

**Kichocheo cha Kimaumbile au Umbo**

Hiki ni kichocheo kinachotumika sana katika kamusi ya KKS katika maelezo mengi ili kujaribu kuwapa wasomaji uelewa wa maumbile, mkao na umbo la nje la samaki anayehusika. Kwa mujibu wa Wilson na Sperber (1995) tunaweza kusema kuwa hiki ni kichocheo cha kimsingi katika maelezo ya kamusi ambacho hutumiwa kurahisisha shughuli ya kufasiri na hatimaye kuelewa kinachoelezwa kwa kukitajirisha na kutafuta athari za kiutambuzi bila kumsababishia mfasiri gharama ambayo ni tatizo kubwa katika shughuli nzima ya ufasiri. Kwa mfano, samaki aina ya *sato* anaelezwa ifuatavyo:

> ….samaki wa maji baridi anayefanana na perege lakini mkubwa zaidi, mwenye magamba na rangi ya kijivu. (KKS 2014:503)

Maelezo ya umbo yanaaminika yanampambanua *sato* na kumfanya kueleweka na mtumiaji wa kamusi asiyemjua samaki huyo. Ni maelezo ambayo huwa kichocheo cha kumwelewa *sato*. Hebu tuangalie vilevile namna mkakati huu unavyotumiwa kama kichocheo cha kumweleza *nguru*. *Nguru* anaelezwa kuwa,

> Samaki mkubwa mrefu wa maji ya chumvi mwenye umbo la mviringo, rangi ya kijivu mgongoni na nyeupe tumboni. (KKS 2014:434)

Ukubwa, urefu na umbo la mviringo ni baadhi ya sifa za kimaumbile au vichocheo vilivyotumiwa kumweleza *nguru* na kusaidia kujenga kiwango fulani cha uhusiano wa kifasiri. Inaaminika maelezo haya yatamsaidia msomaji kumfahamu *nguru* na hata akimwona sokoni anaweza kumtambua kwa kuzingatia vipengele au vichocheo vilivyotumiwa kumweleza. Samaki wengi k.v. *nduwari* ameelezwa kwa kutumia kichocheo cha urefu, naye *sangara* kama *chewa*, ameelezwa kuwa na mdomo mpana. Samaki wengine k.v. *shanuo* ni wa umbo la mviringo na mwenye miiba na wameelezwa kwa kutumia vichocheo hivyo. Mara nyingi kunatumika zaidi ya kichocheo kimoja ili kurahisisha shughuli ya kutafuta athari za kiutambuzi. Lakini inaonekana kichocheo hiki cha kimaumbile ndicho bora zaidi kwa kuwa aghalabu ndicho kinachotumika zaidi.

**Kichocheo cha Makazi**

Mbali na kichocheo cha kimaumbile ni kichocheo cha makazi ambacho kimetumiwa sana na KKS kuwaeleza samaki tofauti tofauti ili kufanikisha utambuzi. Kwa mfano, *nguru* anaelezwa kuwa samaki wa maji ya chumvi. *Pono* pia

anaelezwa kuwa samaki wa bahari, kwa maneno mengine ni samaki wa maji ya chumvi. *Kambare* naye anaelezwa ifuatavyo:

> Samaki wa mtoni au ziwani mwenye masharubu na kichwa bapa. (KKS, 2004: 189)

Licha ya kichocheo cha kimaumbile kunatumika kichocheo cha kimazingira anamokaa *kambare* kumweleza yaani, mtoni au ziwani kinyume na samaki wa baharini. Hii inamsaidia mfasiri wa maelezo kuangalia katika ensaiklopidia ya samaki kujaribu kumtambua samaki huyu na wengine walioelezwa kwa kutumia kichocheo hiki cha kimazingira. Pia mazingira yanatumika kama kichocheo cha kumweleza *kambaremamba* kwa kusema "ni samaki wa maji baridi". Itakumbukwa kuwa katika maelezo ya *kambare* na *kambaremamba*, makazi au aina ya maji wanamokaa yamesisitizwa kama kichocheo cha wazi na hili limelengwa kuongeza kiwango cha kiuhusiano. Kumbuka kuwa kichocheo hiki cha kimazingira kinasisitizwa na hii ndiyo sababu kinatangulia katika maelezo ya *kambaremamba*. Hata katika maelezo ya *pono*, sifa ya anamokaa inatangulizwa ili kuonyesha msisitizo huo. *Kuyu* naye, ni samaki anayepatikana kwenye mikondo ya maji mengi mno. Ni samaki anayepaswa kueleweka kwa misingi hiyo ya makazi yake.

**Kichocheo cha Rangi**

Licha ya sifa za kimaumbile kama urefu, wembamba na upana, kichocheo cha rangi kimetumika sana katika Kamusi ya KKS kuwaeleza samaki. *Kitatange* anafafanuliwa na kupewa sifa za rangi ifuatavyo,

> Samaki mdogo wa umbola duara, mwenye rangi ya manjano iliyochanganyika na nyeupe .... (KKS 2014:248)

*Kitatange* basi hutambuliwa kwa rangi ya manjano na nyeupe. Licha ya kichocheo cha umbo *pono* pia ni samaki mwingine ambaye ameelezwa vilevile kwa kutumia kichocheo cha rangi. *Pono* anaelezwa kuwa:

> ….mwenye umbo la mviringo na rangi mbalimbali, agh. za kijani, buluu au kijivujivu. (KKS 2014: 465).

Samaki mwingine anayetambuliwa kwa kichocheo cha rangi ni mkunga. *Mkunga* anaelezwa kuwa:

> samaki mrefu mwenye umbo la nyoka, huwa na rangi mbalimbali kv. nyeusi, mabatobato ya chui, kijivu au kahawia. (KKS 2014: 356)

*Mkunga* kama *kitatange*, *pono* na samaki wengine wengi wanatambuliwa kwa rangi zao kama kichocheo cha kusaidia kuwatambua katika ensaiklopidia ya samaki. Kichocheo hiki pamoja na vingine humfanya mfasiri kuwaelewa samaki hawa kwa urahisi. Maelezo ya kamusi kwa mujibu wa Unger (2001), yanachukulia kiwango cha kutosheleza cha uhusiano na kwa hivyo, kulenga katika kumtosheleza msomaji kutokana na maelezo yaliyotolewa.

**Kichocheo cha Tabia**

Tabia ni kichocheo kingine cha kiutambuzi ambacho kimetumika katika KKS. Samaki wana tabia mbalimbali. Tabia au mwenendo basi, mbali na sifa nyinginezo, hutumiwa kama kichocheo cha kusaidia katika kuwatambua samaki husika. *Kibua*, ameelezwa kitabia kwamba:

> … huwa juu ya maji zaidi kuliko kuzama chini (KKS 2014: 211)

*Pono* anaelezwa kitabia kuwa:

> … huwa katika hali ya utulivu kama kiumbe aliyelala. (KKS 2014:474)

*Totovu* anaelezwa kwa misingi hii ya kitabia na pia kuwa:

> ni samaki wa jamii ya bangu ambaye akiguswa huvimba. (KKS 2014: 573)

*Kitatange* naye kwa upande mwingine, anaelezwa kuwa ni mwenye tabia ya kuwasakiza wenzake kwenye mtego kisha yeye akatoroka. Tabia za baadhi ya samaki zimekuwa ni kichocheo muhimu cha kuwaeleza ili kupata ufahamu wa haraka hasa wa samaki hawa wanapotazamwa katika muktadha wa samaki wengine. *Mkizi* huelezwa kitabia vilevile kama ni samaki arukaye akiwa na hasira na hata *samsuri* huelezwa kama samaki wa kuruka akiwa majini.

Tabia ya kuruka ni sifa mojawapo inayowabainisha *mkizi* na *samsuri* kama aina ya samaki. Kichocheo hiki pamoja na vingine vinanuiwa kumsaidia mfasiri kutafuta samaki hao katika ensaiklopidia ya samaki na kupata kuwaelewa. Hii ni kwa kuwa mfasiri wa ujumbe anapima maelezo hayo au kichocheo hicho kwa misingi ya tabia za samaki wengine ili kuwaelewa hawa waliolengwa.

**Kichocheo cha Ufananishaji**

Kwa njia mbalimbali kichocheo cha rangi ni sawa na kile cha umbo lakini pia ni tofauti kwani kufanana hakujikiti tu katika umbo, bali huweza pia katika tabia, harufu au hata sifa nyinginezo. Baadhi ya samaki huelezwa na KKS kama samaki wa jamii fulani fulani. Mfano, *totovu* anaelezwa kama samaki wa jamii ya *bangu*. *Nduwari* anaelezwa kuwa samaki wa jamii ya *mzia*. *Kibua* naye anaelezwa kama samaki wa jamii ya *kolekole*.

Inaaminika kuwa kuwahusisha samaki hawa na jamii mbalimbali za samaki kunatosheleza kusaidia ufasiri au kuwafananisha *kambare* na *kambaremamba* kutasaidia kuwapambanua na kuyaweka maelezo yao wazi au kwa maelezo mengine, kuimarisha kiwango cha kiuhusiano kwa wasomaji ili kuwe na kiwango kikubwa cha athari za kiutambuzi wakati wa kufanya ufasiri.

**Kichocheo cha Harufu**

Baadhi ya samaki wameelezwa kwa msingi wa harufu yao au vumba lao. Kwa mfano, *kangaja* anaelezwa na KKS kama:

> aina mojawapo ya samaki mwenye vumba kali. (KKS, 2014: 192).

*Vumba* au harufu kali imetumiwa kama kichocheo cha kumweleza samaki huyu wa baharini. Katika maelezo haya vigezo vingine havikutiliwa uzito sana bali harufu kali aliyo nayo samaki huyu kwani sifa hii ndiyo inayowekwa mbele. Kichocheo hiki si maarufu sana katika kuwaeleza samaki wengine. Labda kwa kuwa hakina uwezo wa kuwa na uhusiano mkubwa na kusaidia katika utambuzi wa maelezo yanayotolewa kwa vile samaki wote wana harafu ya vumba.

**Kichocheo cha Picha**

Kwa sababu ya ugumu wa kuelezwa samaki hasa kwa watu ambao hawana mazoea na mazingira ya mito, maziwa au bahari, picha zimetumika pia kama kichocheo cha kusaidia katika ufasiri. Baadhi ya samaki ambao picha zao zimechorwa ni *dagaa, totovu, kibua, sato, ngisi, pweza, mzia, mkunga, kambaremamba, kijogoo*, n.k.

Kichocheo hiki cha kuwachora samaki kitawawezesha samaki hao kueleweka zaidi, hasa kwa watumiaji wa kamusi ambao hawajawahi kuwaona samaki husika. Picha kama kichocheo inamsaidia msomaji kumwelewa mara moja yule samaki anayelengwa. Kichocheo hiki kinasaidia pia wakati msomaji anamfahamu samaki huyo katika lugha nyingine tofauti. Anapomwona katika picha ndipo anapokumbuka kuwa anamfahamu yaani kwa maneno mengine, anatumia muktadha wake wa elimu awali katika kumwelewa zaidi. Picha ina kiwango kikubwa cha uhusiano labda kuliko vichocheo vingine na humsaidia mfasiri kutafuta athari za kiutambuzi kwa haraka zaidi. Lakini changamoto ya picha ni kuwa, lazima ichorwe kwa ustadi na pengine iwe ya rangi ili ipate kueleweka vizuri.

**Kichocheo cha Vyakula**

Samaki wengine wameelezwa kwa kutumia kichocheo cha vyakula wanavyokula. Vyakula vinalengwa kutumiwa kama mbinu ya kumweleza samaki wa aina nyingine. Kwa mfano, *nguva* anaelezwa kuwa:

> Mnyama mkubwa wa baharini anayekula mwani na anayenyonyesha watoto wake na umbo lake limefanana na binadamu. (KKS 2014: 437).

Ili kumwelewa samaki huyu barabara vichocheo vipatavyo vitatu vimetumika. Kichocheo cha maumbile, cha makazi na hatimaye, kichocheo cha chakula cha *nguva*. Samaki huyu ambaye wakati mwingine huitwa mnyama *tuhula* na kwamba hula majani ya baharini, yaani *mwani*. Tukumbuke kuwa mkakati wa vyakula hautumiwi sana katika kamusi hii. Hata hivyo, katika kamusi hii kichocheo hiki kinatumika katika kueleza ndege na wanyama wa aina nyingine. Labda kwa kuwa kama kichocheo cha harufu, mkakati huu hauna uwezo wa kujenga uhusiano mkubwa ili kurahisisha ufasiri na ndio sababu kinatumika kwa uchache katika maelezo ya KKS.

**Changamoto za Vichocheo Vinavyotumika**

Katika sehemu hii tunajadili matatizo yanayofungamana na vichocheo mbalimbali. Tunajadili matatizo yanayofungamana na vichocheo vya rangi, maumbile, makao au

makazi, vyakula, makazi na picha; kwa jinsi gani kuna matatizo haya katika mifano fulani na jinsi au namna ambayo matatizo haya yangetatuliwa.

**Changamoto za Kichocheo cha Kimaumbile/Umbo**

Changamoto ya kwanza inahusiana na mkakati wa kueleza samaki kwa kutumia umbo k.v. udogo, ukubwa, urefu, wembamba, ubapa, mviringo n.k. Kwa mfano, *dagaa* anaelezwa kuwa:

Samaki mdogo (KKS, 2014)

Katika maelezo haya, kichocheo hiki kinasisitizwa. Hata hivyo ni vigumu kujua kiwango cha udogo unaozungumziwa. Ikumbukwe kuwa *dagaa* siye samaki wa pekee aliye mdogo. Kuna samaki wengine ambao ni wadogo. Kwa mfano, *kibua* akilinganishwa na *chewa* anaweza kusemekana kuwa ni samaki mdogo. Isitoshe, kichocheo cha umbo pekee katika kueleza *dagaa* ni jambo linalopelekea kutokamilika kwa maelezo. Msemaji anaposema hivi, ubongo hujaribu kupata viathiri vifuatavyo:

a) Huyu ni samaki mdogo
b) Labda anaishi baharini
c) Umbo lake ni dogo kama nini?

Kwa jinsi hiyo, itakuwa vigumu kwa mfasiri kumjua samaki huyu au utamaduni wake kwa jumla kwani atashindwa kuelewa kiasi cha udogo kwa mujibu wa mambo anayoyajua. Kwa mujibu wa Sperber na Wilson (1995), kichocheo hiki kitakataliwa maana kitakuwa kimeshindwa kutosheleza mahitaji ya kiutambuzi. Labda maelezo haya yangeongezewa maelezo zaidi kama vile "ana umbo la kima cha kidole" ili kuafiki zaidi. *Chewa* anapoelezwa kuwa "samaki mkubwa wa baharini" mkakati huu pia unakuwa na matatizo kwani kuna samaki wengine baharini ambao ni wakubwa kama *papa* na walio na vinywa vipana pia. Ni vigumu kichocheo cha ukubwa na udogo kutumika kwa ukamilifu kuwaelezea samaki walio katika jamii inayoandikiwa kamusi na kwa kiwango kikubwa ni kichocheo hafifu.

**Changamoto za Kichocheo cha Kiufananishi**

Kama tulivyotaja hapo awali, baadhi ya samaki wamefananishwa na samaki wengine. Kwa mfano, *kambare* na *kambaremamba*. *Totovu* ameelezwa kuwa ni wa jamii ya *bangu*, na kwa hivyo kufananishwa naye. *Nduwari* naye ameelezwa kuwa samaki wa jamii ya *mzia* na *ngagu* wa jamii ya *changu*. Kufananisha huku kunalenga katika kumfanya msomaji kumwelewa samaki anayeelezwa vizuri zaidi.

Kutokana na maelezo yaliyotolewa kuhusu msamiaji wa samaki, changamoto kadha zaelekea kuibuka. Kwanza, inachukuliwa kuwa samaki anayetolewa maelezo, kama vile *totovu* ambaye ni samaki wa jamii ya *bangu,* ni lazima msomaji awe anamfahamu *bangu* ili kumwelewa *totovu*. Vivyo hivyo, ni sharti unamfahamu samaki aina ya *mzia* ili umhusishe na *nduwari*. Samaki wote wawili wanaweza kuwa samaki wageni kabisa kwa msomaji, hivyo basi kuibua changamoto katika kuwatambua samaki husika. Mkakati huu unasaidia tu pale ambapo kuna samaki wa

kawaida sana ambaye anajulikana na watu wengi ambao ni watumiaji wa kamusi ili kumfananisha na samaki anayeelezwa.

**Changamoto za Kichocheo cha Rangi**

Mkakati huu wa rangi umetumika sana. Ni kweli samaki wengi wana rangi zinazoweza kuwatambulisha kwa urahisi na haraka. *Kambi* anaelezwa kuwa ni mwenye rangi inayofanana na rangi ya maji anamokaa.

Kwa kweli si rahisi kuyaelewa maelezo haya. Labda ina maana kuwa hubadilisha rangi yake ili kuingilianana maji anamokaa. Maji yana rangi gani au ipi? Ndio baadhi ya maswali tunayojiuliza tunapokumbana na maelezo haya. *Pono* anapoelezwa kuwa na rangi “mbali mbali” baadhi ya rangi hizi zikiwa kijani, samawati au kijivujivu inakuwa vigumu kutumia rangi kumwelewa samaki kama *pono*. Rangi ya kijivujivu ni rangi ya asilimia kubwa ya samaki kwa hivyo, haisaidii katika kuwatambua na kuwaeleza samaki. *Mkunga*, kama samaki ni mgumu kumwelewa kwa kutumia rangi. Hii inatokana na sababu kwamba rangi zenyewe ni nyingi na zile ambazo tunapewa ni mifano michache tu. Kichocheo cha rangi ni kizuri maana kuna samaki wengine wa kikahawia, wengine weusi lakini wengi ni wa kijivu. Hata hivyo, wale samaki ambao rangi zao hazifanani hata kama wamo katika familia moja inafaa waelezwe kwa kutumia vichocheo vingine madhubuti zaidi. Aidha, ikumbukwe kuwa rangi za samaki ni nyingi. Kuna zile zilizokolea na nyingine hazikukoleza. Lakini sifa hii ya kukoleza na kutokoleza haitumiki katika kuzipambanua rangi hizi katika KKS.

**Changamoto za Kichocheo cha Harufu**

Imeelezwa kuwa samaki aitwaye *kangaja* ana harufu kali. Lakini inavyojulikana kwa mfano, *kambaremamba* ana vumba kali pia. Ukali wa vumba unawategemea watu binafsi. Watu wasiokuwa wavuvi huona vumba la samaki ni kali zaidi, lakini wavuvi na wachuuzi wa samaki na hasa wabichi, wanaweza kuvumilia. Kichocheo hiki cha harufu kimefanya maelezo ya KKS kuwa dhaifu zaidi na hasa yale yanayofungamana na samaki. Hata kama hutumika na vichocheo vingine hakisaidii sana kuongeza au katika ufasiri na hatimaye uelewa wa samaki anayelengwa kwa msomaji.

**Changamoto za Kichocheo cha Picha**

Picha ni kichocheo kizuri sana cha kimaelezo na huweza kuwasaidia watu ambao hawamjui samaki fulani vizuri ili wapate kumjua. Kwa mfano, picha zinawatenga *ngisi* na *pweza* vizuri katika kamusi ya KKS. Lakini kuna samaki waliokaribiana katika maumbo yao k.v. *samsuri* na *chuchunge* kiasi cha picha kutoweza kusaidia. Inakuwa vizuri samaki hawa kupigwa picha ili waonekane hata kwa namna iliyo bora zaidi na kupambanua maelezo yao. Kwa mujibu wa nadharia ya uhusiano picha ya *samsuri* si kichocheo mwafaka cha kumpa mfasiri uwezo wa kutafuta athari za kiutambuzi na kuishia kufanya uteuzi wa ufafanuzi ufaao. Aina za picha ya *pandu* na *cheche* hazitofautiani hivi kwamba kigezo cha picha hakina msaada

mkubwa sana lakini lazima tuseme kichocheo hiki ni bora hasa ikiwa wanaolengwa ni watoto.

**Changamoto za Kichocheo cha Makazi**

Kigezo cha kueleza makazi ya samaki ikiwa ni wa mtoni, baharini au ziwani humpa mtu habari fulani kumhusu samaki aliyelengwa, yaani kuhusiana na anakoweza kupatikana. Hata hivyo, ni kichocheo chenye changamoto nyingi. Kwanza, hakimsaidii sana msomaji kumwelewa samaki huyo vizuri tofauti na samaki wengine. *Pono* anaelezwa kama samaki wa baharini ambaye hupenda kukaa mahali palipo na mwani. Mbali na kichocheo hiki vinatumika vichocheo vya rangi na umbo kumweleza *pono*. Kama anavyosema Zgusta (1971), wanaleksikografia hutumia sifa za kubainisha maelezo yao kwa kiasi kikubwa wakimlenga msomaji wa kawaida. Kigezo hiki kinakuwa hafifu zaidi kinapotumika bila kuambatana na vigezo vya umbo vilivyo dhahiri kama ilivyo katika maelezo haya ya chewa:

> namna mojawapo ya samaki wa baharini....(KKS, 2014)

Ni kweli lakini pia samaki wengine ni wa baharini. Kwa mfano, *chafi* au *tafi* ni samaki wa baharini pia. Kwa kisai kikubwa kichocheo hiki hakimsaidii sana msomaji kwa kuwa samaki wengine wote ni wa baharini au ziwani au hata mtoni. Vile vile hata kichocheo cha umbo la *chewa* hakimsaidii mtumiaji wa KKS kwa kuwa upana wa kinywa cha samaki si kichocheo ambacho kitasaidia katika ufasiri wa haraka na usio na gharama/tatizo kubwa. Katika hali kama hii waandishi wa maelezo walipaswa kufikiria kichocheo mwafaka au hata kuongeza idadi ya vichocheo ili kufanikisha maelezo yao kwa msomaji.

Lazima ikumbukwe kuwa samaki wote hukaa majini na kichocheo hicho hakina uzito wa kutosha. Pia katika maisha ya kisasa, samaki wengi wametolewa katika maji yake asilia na kufugwa au kukuzwa vidimbwini au hata mitungini.

**Changamoto za Vyakula**

Kichocheo cha vyakula kimetumika katika kamusi ya KKS kuelezea viumbe wengine k.v. *batabukini*. Kinatumika mara chache sana katika kamusi ya KKS kuwaelezea samaki. Mfano, tuliourejelea ni wa *nguva* ambaye inasemekana anakula *mwani*. Kichocheo hiki cha maelezo kimetumika pamoja na vigezo vya umbo na tabia. Waandishi wa kamusi hawana uhakika kuhusu ni samaki wangapi hula mwani na pia chakula kingine cha *nguva*. Samaki wengi hula mseto wa vyakula, kwa hivyo kutumia vyakula kumweleza samaki ni jambo ambalo kwa mujibu wa Wilson na Sperber (2004) si kichocheo kamili cha kiutambuzi cha kumsaidia msomaji kumwelewa samaki huyu kisawasawa. Hata hivyo, kwa kuwa ishara nyingine k.v. umbo na tabia zimetumiwa, basi labda vinaweza kusaidia kumwelewa samaki huyu.

**Changamoto za Kichocheo cha Tabia**

Kuna baadhi ya samaki ambao wametambulishwa kwa kuwahusisha na tabia za kipekee wanapolinganishwa na samaki wengine. Kwa mfano, *kibua* ambaye tumemrejelea hapo juu, ameelezwa kuwa anapenda kuelea juu ya maji. Itakumbukwa kuwa samaki wengi wana tabia hii ya kuelea juu ya maji hasa wanapokula. Kwa mfano, hata *sato* aghalabu hupenda kuelea juu ya maji. *Pono* naye ameelezwa kuwa huwa mtulivu kama aliyelala. Ni kweli kwamba samaki wengi kama hawakushtuliwa huweza kutulia majini wakawa kama waliolala. Labda ingekuwa bora utulivu huu ukaelezwa ni wa kiasi gani ili kuwa kichocheo cha kuufanya ufasiri wa samaki husika kuwa bora zaidi. Kwa mujibu wa nadharia ya uhusiano, kichocheo hiki hakitoshelezi katika kuutajirisha uwezo wa msomaji wa kuyaelewa maelezo ya samaki husika.

**Hitimisho**

Kazi hii iliazimia kuvieleza vichocheo vya kimaelezo vinayotumiwa na kamusi ya KKS. Ili kufanikisha hayo, tulitumia nadharia ya kiuhusiano ya Dan Sperber na Deirdre Wilson (1995). Imebainika kuwa kamusi ya KKS imetumia vichocheo kama vile vya tabia, chakula, malazi, rangi, umbo, vumba, na hata picha kufananisha ili kumfanya samaki husika aeleweke na msomaji. Vichocheo vingi vimetumiwa kwa pamoja ili kuongeza uhusiano wa kimaelezo na kufanya kazi ya kutafuta viathiri vya kiutambuzi vyenye kiwango cha juu. Hata hivyo, kuna baadhi ya samaki walioelezwa kwa kutumia kichocheo kimoja dhaifu na kufanya uteuzi wa maana moja iliyolengwa kuwa ngumu. Pia kuna hata samaki kadha ambao wameelezwa kwa vichocheo vingi na baadhi yavyo havina nguvu ya kurahisisha suala na jukumu la ufasiri ambalo ndilo la kimsingi katika nadharia ya kiuhusiano. Ingelikuwa bora zaidi iwapo vichocheo vingeongezwa au kukatumika vichocheo ambavyo vingefanikisha utambuaji wa samaki anayeelezwa kwa njia bora zaidi.

**Marejeleo**

Blakemore, D. (1992). *Understanding Utterances*. Oxford: Blackwell.

Carston, R. (1988). "Implicature, Explicature and Truth-theoretic Semantics"Katika R. Kempson (ed) uk. 155-188.

Grice, P. (1975). "Logic and Conversation" katika P. Cole na I. Morgan (eds) *Syntax and Semantics 3.* New York: Academic Press. pp 41-58.

Grice, P. (1989). *Studies in the Way of Words*. Cambridge MA: Harvard University Press

Marmaridou, S. A. (2000). *Pragmatic, Meaning and Cognition.* Amsterdam, John Benjamin. Oxford: Blackkwell, pp. 607-632.

Sperber, D. (1996). *Explaining Culture*. Oxford: Blackwell.

Sperber, D. na Wilson, D. (1995). *Relevance Theory*. Oxford: Blackwell.

TATAKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Unger, C. (2001). *On the Cognitive Role of Genre: A Relevance - Theoretic Perspective*. Unpubslihed PhD Thesis, University of London.

Wilson, D. & Sperber, D (2004). "Relevance Theory" katika Horn, L. & Ward, G. (Eds.). *The Handbook of Pragmatics.* p.p. 633-657. Oxford: Blackwell.

Zgusta, L. (1971). *Manual of Lexicography*. The Hague: Mouton.